

# NAFASI YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO KATIKA UFUNDISHAJI WA KISWAHILI KAMA LUGHA YA KIGENI

*Sarah Ndanu M. Ngesu*  
*Chuo Kikuu cha South Eastern, Kenya*

## **Utangulizi**

Matumizi ya TEHAMA katika makala hii yanahusu uwezo wa kutumia chombo au kifaa chochote cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (kuanzia sasa, TEHAMA) katika kufundishia lugha za kigeni (kuanzia sasa, LG) kama vile Kiswahili. Kwa mujibu wa wataalamu Johan (1992), Maw (1999), Safari (2012) Kramch (2014), Mohochi (2016) na Michira (2017) kwa miaka 10 iliyopita, ulimwengu umeshuhudia matumizi makubwa ya teknolojia ambayo yana athari hasi katika ufundishaji wa lugha za kigeni. Aidha, maendeleo katika jamii kwenye karne hii ya 21 yanahimiza kuwapo kwa ubunifu katika mchakato wa ufundishaji unaotilia maanani utangamano wa wanafunzi wote duniani.

Ufundishaji wa lugha katika sehemu nyingi duniani hukabiliwa na changamoto kama vile ukosefu wa walimu waliofuzu, ukosefu wa vitendea kazi pamoja na kutokubalika kwa mbinu nyinginezo za ufundishaji (Mathew, 1992). Kulingana na Bilyalova (2017), njia mojawapo ya kukabiliana na changamoto za ukosefu wa walimu wa kutosha, ukosefu wa vitendeakazi vya ufundishaji na matumizi ya

mbinu changamani katika ufundishaji wa lugha za kigeni ni matumizi ya TEHAMA. Altun (2015) kuhusu suala hili anaeleza kwamba TEHAMA ni zana muhimu katika ufundishaji kwa kuwa huwapa motisha wanafunzi na kulifanya somo kufunziwa na wanafunzi wote.

Kwa mujibu wa Shin (2015), maendeleo ya teknolojia yamepanua matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa lugha, Katika karne hii ya 21 walimu wa lugha wanatakiwa kuwa na uelewa wa kutumia TEHAMA kama vile kompyuta na mtandao kama mbinu ya ufundishaji ili kufanikisha ufundishaji wa LG. Nchi mbalimbali kama vile Korea zimeanzisha programu za kuwafundisha walimu wa lugha jinsi ya kutumia kompyuta ambayo ni kipengele kimojawapo cha TEHAMA katika ufundishaji wa lugha ya Kiingereza (Shin, *keshatajwa*).

Mohochi (2016) katika utafiti aliofanya kuhusu ufundishaji wa Kiswahili kupitia teknolojia anaeleza kwamba mbinu hii haijapewa nafasi inayostahiki. Aidha, Mohochi anasema kuwa lugha za nje kama vile Kijapani, Kifaransa, Kichina na Kijerumani hufundishwa kwa upana kidijiti kuliko lugha za Kiafrika kikiwamo Kiswahili. Isitoshe, programu nyingi za vyuo vya walimu zimetambua umuhimu wa kutumia TEHAMA katika ufundishaji wa LG. Vifaa vya TEHAMA vinavyoweza kutumiwa katika ufundishaji wa Kiswahili ni kama vile: kompyuta, mtandao, televisheni, simu za kiganjani, redio na kadhalika. Hata hivyo, makala hii imeshughulikia ufundishaji unaokitwa kwenye kompyuta.

Lengo la makala hii ni kufafanua nafasi ya TEHAMA kama nyenzo muhimu katika ufundishaji wa Kiswahili ikiwa lugha ya kigeni. Ingawa historia ya matumizi ya teknolojia kama vile tarakilishi katika ufundishaji wa lugha za Ulaya ni ya kitambo, Auer na wenzake (2017) wanaeleza kwamba teknolojia haijatumiwa inavyostahili katika ufundishaji wa lugha. Kuhusu lugha ya Kiswahili, Michira (2017) na Mohochi (2016), wanaeleza kwamba ufundishaji wa Kiswahili kama LG kwa kutumia teknolojia umepewa nafasi ndogo. Kwa mfano,